**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA HAI**
**SHULE YA SEKONDARI HARAMBEE**

S.L.P. 6633,
MOSHI
Tarehe: 29-04-2019

Namba za simu
Mkuu wa shule: 0784683414/ 0755755991
Makamu Mkuu wa shule: 0753380229/0714 731 006
Matron / Patron: 0756284171

Ref. No: HSS/FS/JI/Vol 1/03
Mzazi/ Mlezi wa mwanafunzi..........................................................................
S.L.P..................................................
..........................................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA HARAMBEE HALMASHAURI YA HAI MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2019.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii **mwaka 2019/2020** tahasusi ya ............. Shule ya **Sekondari HARAMBEE** ipo umbali wa kilometa 25 Magharibi mwa mji wa **MOSHI**. Usafiri wa basi kutoka mjini MOSHI unapatikana katika kituo cha mabasi **MOSHI MJINI** na nauli ni shilingi **elfu moja tu(1000/=),** na utashuka kituo cha **NSHARA UFUNDI** au **HARAMBEE SEKONDARI.**

**Muhula wa masomo unaanza tarehe 08-07-2019**. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 08-07-2019, na mwisho wa kuripoti ni tarehe **22-07-2019**.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare ya shule.**

I. Sketi **mbili (02)** za marinda ya kawaida za rangi ya zambarau iliyokolea(dark purple) ndefu na zinazovuka magoti

II. Mashati **mawili(02)** meupe ya mikono mirefu ( Tetron)

III. Rangi ya Hijab (kijuba) ifanane na rangi ya shati (nyeupe)
IV. Nguo za michezo ni track suit ya rangi ya kijivu

V. Viatu vya shule hii ni vyeusi vya kufunga na kamba vya ngozi na visigino vifupi.

VI. Soksi jozi mbili (02) nyeupe

VII. Sweta mbili (02) inayofanana na rangi ya sketi

VIII. Nguo za kushindia (shamba dress) mbili mshono aina ya solo, kitambaa cha drafti ndogo ya rangi ya brown yenye zipu nyuma , kola ndogo na mikanda miwili nyuma, iwe ndefu inayovuka magoti. Kwa waislamu hijabu (kijuba) cha rangi ya brown inayofanana na nguo ya kushindia.

IX. Tai ndogo aina ya kipepeo (Neck Tie) inayofanana na rangi ya sketi.

X. T-shirt ya rangi nyeupe isiyo na maandishi yoyote wala urembo .

XI. Raba na Soksi kwa ajili ya michezo. Soksi ziwe za rangi nyeusi/bluu za mistari ya rangi nyeupe
**NB:** Mchoro wa sketi na shamba dress vimeambatanishwa katika kiambatanishi A mwishoni

### 2.2 Ada na michango ya shule.

(A) **Ada ya shule** kwa mwaka ni shilingi 70,000/= (Sabini elfu tu). Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000/= (thelathini na tano elfu tu) kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha za Ada tu zilipwe kwenye akaunti ya shule **40101200094** katika benki ya **NMB.** Jina la Akaunti ni **HARAMBEE SECONDARY SCHOOL** (tafadhali andika jina kamili la mwanafunzi, kidato pamoja na tahasusi yake kwenye pay in slip).

(B) **Mchanganuo** wa michango mingine imefafanuliwa kwa mihula kama inavyoonekana katika jedwali linalofuata:-

| S/N | KIPENGELE | KIASI KWA MUHULA WA I | KIASI KWA MUHULA WA II |
|---|---|---|---|
| 01 | Ukarabati wa samani | 15,000/= | |
| 02 | Kitambulisho na picha | 6,000/= | |
| 03 | Taaluma | 10,000/= | 10,000/= |
| 04 | Wapishi, Walinzi na vibarua wengine | 15,000/= | 15,000/= |
| 05 | Nembo ya shule | 2,000/= | |
| 06 | Huduma ya kwanza | 5,000/= | |
| 07 | Bima ya afya | 5,000/= | |
| 08 | Mitihani ya kujipima (Mock) | 20,000/= | |
| 09 | Fedha ya tahadhari | 5,000/= | |
| | JUMLA | 83,000/= | 25,000/= |

**Angalizo**: (a) Jumla ya Ada na michango mingine yote kwa mwaka ni **Tsh. 178,000/=**
(b) Jumla ya Ada na michango mingine yote kwa nusu mwaka (**Muhula) ni Tshs. 118,000/=**
(c) Michango mingine yote isiyo ya Ada ilipwe kwenye Akaunti Namba **40102300335** Jina la Akaunti ni **HARAMBEE SECONDARY SCHOOL**
(d) Kama mwanafunzi ana Bima ya Afya aje nayo na asilipe fedha ya bima

(C) **Mahitaji mengine ya kitaaluma**

(i) Nakala ya matokeo ya kidato cha nne (copy of result slip)

(ii) Nakala ya cheti cha kuzaliwa (copy of birth certificate)

(iii) Mathematical Set kwa tahasusi zote na Scientific Calculator aina ya fx 991 original kwa tahasusi ya HGE tu.

(iv) Begi la kubebea madaftari na vitabu ( pochi haziruhusiwi kamwe)

(v) Counter books kumi (10) – Quire three kwa ajili ya masomo darasani

(vi) Madaftari madogo kumi na mbili (12) kwa ajili ya mazoezi darasani.

(vii) Kalamu za wino nyeusi au bluu , penseli za kutosha, na ruler ya sentimeta thelathini (sm 30)

(viii) Ream moja A4 (Photocopying papers)

(ix) Vitabu vya masomo ya History, Geography, Kiswahili, English language na Economics katika tahasusi za HGK, HGL na HGE

(x) Graph papers

(xi) Advanced Learner's Dictionary (Oxford)

(D) **Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni**.

(i) Godoro inchi mbili na nusu (2.5")

(ii) Mashuka jozi mbili rangi ya pink

(iii) Blanketi moja zito (Kuna baridi kali sana)

(iv) Foronya mbili za rangi ya pink

(v) Chandarua moja ya duara (nyeupe)

(vi) Sanduku moja imara la bati (tranka)

(vii) Begi la kusafiria lenye kufuli

(viii) Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli, kijiko, kikombe)

(ix) Buti za mvua

(x) Mwamvuli

(xi) Toilet paper
(xii) Sweta nyeusi mbili za kuvaa baada ya masomo, zisiwe na maandishi wala urembo. Zenye kofia pia zinaruhusiwa
(xiii) Taa ndogo ya solar au tochi (ikiwa umeme utakatika)
(xiv) Kanga jozi mbili (02), taulo moja na nguo ndani za kutosha, mafuta ya kujipaka na chanuo.
(xvi) Mahitaji mengine binafsi ya kike

**NB. Vyakula haviruhusiwi kabisa kuja navyo shuleni**

**E. VIFAA VYA USAFI**

| Namba | Aina ya Kifaa | Tahasusi husika |
|---|---|---|
| 1. | Ndoo za kufanyia usafi mbili | Wote |
| 2. | Brush ngumu yenye mpini(hard broom) | HGK |
| 3. | Fagio la chelewa | Wote |
| 4. | Squeezer na mpini | HGK |
| 5. | Brush za kusugulia vyoo | Wote |
| 6. | Rato imara na mpini wake(England) | HGL |
| 7. | Panga imara lililonolewa | Wote |
| 8. | Fyekeo imara lililonolewa | Wote |
| 9. | Jembe kubwa lenye mpini lililonolewa | Wote |
| 10. | Reki yenye mpini | HGE |
| 11. | Fagio laini na mpini | HGE |
| 12. | Fagio refu la kuiondolea buibui | wote |

**3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

(i) Wizi

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini (90) bila taarifa / utoro

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu /walezi na jamii kwa ujumla

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule .

(vi) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.

(vii) Uvutaji wa sigara, kutafuna mirungi au kuvuta ugoro.

(viii) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja,(usagaji) au kuolewa.

(ix) Kupata au kutoa mimba.

(x) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
(xi) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
(xii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi au line ya simu katika mazingira ya shule.

(xiii) Kudharau bendera ya Taifa

(xiv) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

(xv) Uharibifu wa mali ya Umma, miundo mbinu ya shule au mali za wanafunzi wenzake kwa makusudi

**NB: Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shule.**

**4. Viambatanisho na Fomu Muhimu**

(i) Fomu ya Uchunguzi wa Afya ya mwanafunzi (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali

(ii) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi /mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai

(iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada na michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

(iv) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu

**5. Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo yote na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**
Saini ya Mkuu wa Shule.................................................
Jina la Mkuu wa Shule **MUHOCHI F. T**
Mhuri wa Mkuu wa Shule......................................

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI HARAMBEE
S. L. P. 6633 — MOSHI

*Harambee Secondary School*
*P. O. Box 6633, Moshi. Mobile 0784683414/0755755991*

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

**HABARI ZA MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi ...................................................
2. Tarehe ya kuzaliwa ......................................................
3. Mahali alipozaliwa: Mkoa ........................................ Wilaya ....................................
Tarafa ........................... Kata.................................. Kijiji/Mtaa ..................................
4. Dini .........................5. Dhehebu.................................. Kabila ..................................

**HABARI ZINAZOWAHUSU WAZAZI/WALEZI**

1. Jina la baba mzazi/mlezi............................................................. Anuani................................
.......................................... Namba ya simu ya kiganjani.................................... Simu ya Ofisini.............................. Kazi ya baba mzazi/mlezi.................................... Yuko hai? Ndiyo/Hapana (Kata isiyohusika)

2. Jina la mama mzazi/mlezi........................................................ Anuani................................
....................................... Namba ya simu ya kiganjani.................................... Simu ya ofisini.....................................................kazi ya mama mzazi/mlezi................................yuko hai? Ndiyo/hapana(kata isiyohusika)

Picha ya mzazi /mlezi

Picha ya mzazi/mlezi

3. Ndugu wa karibu aliyeidhinishwa na mzazi/mlezi anayeweza kupewa taarifa za matatizo ya mwanafunzi kwa haraka endapo mzazi/mlezi hatapatikana.
Jina kamili ............................................................ Anuani.......................................
Namba ya simu ya kiganjani ................................... Simu ya ofisini ....................................
Kazi yake ................................ Uhusiano na mwanafunzi ...........................................

Picha ya ndugu wa karibu

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**
**SHULE YA SEKONDARI HARAMBEE**
**S.L.P 6633, MOSHI**

# HATI YA UTII WA SHERIA

**A: MWANAFUNZI**

JINA LA MWANAFUNZI.................................................................

TAREHE YA KUZALIWA.............................................................

JINA MZAZI/MLEZI...................................................................

UHUSIANO WA MLEZI (BABA, MJOMBA, KAKA NK)...........................

KAZI YA MZAZI/MLEZI...............................................................

Mimi..............................................................nikiwa mwanafunzi wa shule hii, nakubali kuwa, umma wa nchi hii ya Tanzania ndiyo uliyonipa nafasi hii maalumu ya masomo, ili nimalizapo niweze kuitumikia nchi katika kuleta maendeleo. Hivyo basi ninaahidi kwamba, nitajibidiisha hapa shuleni na pia nimalizapo shule. Ili kutimiza shabaha hiyo, ninakubali na kuahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitatii sheria za shule na amri nitakazopewa na uongozi wa shule(walimu na serikali ya wanafunzi). Nikiwa na malalamiko au maoni nitayafikisha kwa uongozi wa shule kufuatana na utaratibu uliowekwa bila kuogopa chochote.

Tarehe..............................................................saini..........................

**B: MZAZI/MLEZI.**

Mimi Bwana/Bibi.........................................Mzazi/Mlezi wa........................ Nimesoma kwa makini sheria za shule nikiwa na binti yangu kama zilivyoandikwa katika maagizo kwa wazazi na kujadili pamoja nae na amezielewa sheria hizo. Ninakubali kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi ya binti yangu na nitakubaliana na adhabu yoyote itakayoamriwa na shule pale binti yangu atakapokiuka mojawapo ya sheria hizo, na nitashirikiana na shule kuona kuwa mwanangu anazingatia kwa makini kwa manufaa ya Umma. Tarehe.....................Saini........................Namba ya simu..........................

***Harambee Secondary School***
***P. O. Box 6633, Moshi. Mobile 0784683414/0755755991***

## MEDICAL EXAMINATION FORM

**PART I: PERSONAL PARTICULARS** (To be filled by the student)
Surname............................ Other names.......................... ................................
Age ................ Sex............. Combination................ School...............................

**PART II: PERSONAL HISTORY (To be filled in a government hospital by qualified Medical Officer)**

Are you suffering or have you suffered from any of the following? Indicate Yes or No
1. Tuberculosis.................................... 11. Epilepsy.............................
2. Asthma................................................. 12. Deformity..........................
3. Rheumatic fever................................. 13. Mental illness....................
4. Allergic disorders.............................. 14. Eye disorder.......................
5. Heart disease.................................... 15. Ear, Nose, Throat disorder..............
6. Gastric or duodenal ulcers...................... 16. Skin disease........................
7. Jaundice .......................................... 17. Anemia............................
8. Dysentery......................................... 18. Varicose veins...................
9. Kidney disease................................... 19. Diabetes...........................
10. Gynecological disorder........................ 20. Any other serious disorder (specify)...........

**PART III: PHYSICAL EXAMINATION**

1. Height (cm) ..................................
2. Skin...............................................
3. Weight (kg)..................................
4. Eyes: Conjunctive......................... Pupil................. Vision
Right.......................................... Left...................5. Ears (state if any discharge).......................... Mouth/throat.....................................
6. Nose.................................................. Respiratory system...............................
7. Abdomen............................................. Any abnormality.................................
8. Cardiovascular system............................... Blood pressure ..................................
Systolic .................................................. Diastolic..........................................
Heart: Any murmur ..................................... Arteries veins ....................................

**PART IV: LABORATORY**

1. Urine: Albumin................................ Sugar..................... Leucocytes....................
Schistosoma..................... ....................
2. Stool: Special emphasis on hookworms or schistosoma....................................
3. Blood examination
a) Hb level.........................................
b) Neutrophil......................................
c) Eosinophils......................................
d) Basophiles.......................................
e) Lymphocytes....................................
f) Monocytes.......................................
g) ESR.............................................
4. X – Ray examination: Chest (include Radiologist's report)..............................
5. Serology Widal test ....................... VDRL........................................
6. Pregnancy test..............................

**PART V: CONCLUSION**

I have examined Miss.......................................... and consider that she is physically and mentally fit/not fit to be admitted for secondary education.

Name.......................................... Title.........................
Qualification................................. Signature..................... Date...................
Address...........................

KIAMBATANISHO A.



